

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA PILI

06 APRILI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA PILI – TAREHE 06 APRILI, 2022

I. DUA

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI MKUU:

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Tume ya Uratibu na Udhhibiti wa UKIMWI) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

11. MHESHIMIWA JOSEPH KIZITO MHAGAMA (MADABA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itasaidia ujenzi wa Stendi ya Madaba ikizingatiwa kwamba stendi hiyo ipo kwenye eneo la kimkakati.

**12. MHESHIMIWA EMMANUEL PETER
CHEREHANI (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Waziri Mkuu aliyoitoa Mwaka 2017/2018 ya ujenzi wa Kituo cha Afya Ulowa katika Jimbo la Ushetu.

**13. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA
(BUYUNGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Watumishi wa Afya wa Kada mbalimbali katika Wilaya ya Kakonko.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**14. MHESHIMIWA REGINA NDEGE QWARAY (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuchimba Mabwawa ya kuhifadhia maji kwa ajili ya kunyweshea mifugo katika kila Kijiji nchini.

15. MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina kauli gani juu ya ushuru mkubwa wa bidhaa ya ngozi unaotozwa bandarini na vikwazo vya kusafirisha bidhaa hiyo nje ya nchi.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

16. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, nini mkakati wa Serikali kukifanyia ukarabati Kituo cha Polisi cha Nansio.

17. MHESHIMIWA FATMA HASSAN TOUFIQ (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kuna Wahanga wangapi wa vitendo vya Ukatili nchini kuanzia Mwaka 2019 hadi 2022.

18. MHESHIMIWA JERRY WILLIAM SILAA (UKONGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni Sheria gani inasimamia orodha ya wanaostahili kutumia ving'ora na vimulimuli kwa misafara ya Viongozi na Wananchi wa kawaida.

WIZARA YA AFYA:

19. MHESHIMIWA DENNIS LAZARO LONDO (MIKUMI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kuna Wataalamu wangapi wa huduma za utengamao na mazoezi ya viungo (*Physiotherapist*) katika Mkoa wa Morogoro.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

20. MHESHIMIWA DKT. PAULINA DANIEL NAHATO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itatoa vibali kwa Vyuo Vikuu vyenye upungufu wa Wahadhiri ili viweze kuajiri Wahadhiri wapya.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

DODOMA
06 APRILI, 2022

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE